




# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na: 6. Msimu wa Kilimo 2019/20

Tathmini Novemba 21-30, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 1-10, 2019

### Muhtasari


- Katika *dikadi* hii, wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka waliendelea na shughuli za palizi. Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wameendelea na shughuli ya kupanda mazao
- Mvua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho.
- Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo, kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019

**K**atika kipindi cha *dikadi* hii, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha kusogea kwa ukanda wa mvua katika eneo la ukanda wa kusini. Kuimarika kwa wimbi anga “**Madden Julian Oscillation**” katika kipindi hiki kulisababisha kuimarika kwa mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kati mwa nchi. Joto la bahari la wastani liliendelea kuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

### MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019

**K**atika kipindi cha Novemba 21-30, 2019, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua. Kiasi cha mvua cha zaidi ya milimita 100 kilipatikana katika maeneo ya ziwa Viktoria, mikoa ya Manyara, Pwani, Lindi, Ruvuma na Mtwara, kama inavyoonekana katika kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Novemba 21- 30, 2019

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019

**K**atika *dikadi* hii, mvua zilizonyesha katika maeneo yanayopata mvua za Vuli zimesaidia kuimarisha unyevunyevu kwenye udongo kwa shughuli mbalimbali za kilimo. Katika maeneo haya shughuli kuu ilikuwa kupalilia ambapo mazao yameripotiwa kuwa katika hali nzuri. Baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan mikoa ya Kagera na Mwanza, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya jani la tisa. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kama vile mkoa wa Tabora, Rukwa na Kigoma

wakulima wameendelea na shughuli za upandaji wa mazao. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa mzuri katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

### HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2019

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vimeanza kuongozeka katika maeneo mbalimbali ya nchi kutokana na mvua zinazoendelea.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2019.

**K**atika kipindi cha *dikadi* hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha kusogea kwa ukanda wa mvua katika eneo la ukanda wa kusini. Vilevile, kunatarajiwa kuimarika kwa wimbi anga “**Madden Julian Oscillation**” na kusababisha kuimarika kwa mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

### HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2019.

**M**aeneo ya kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa),

kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) kunatarajiwa kuwa na mvua za wastani katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) kunatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

### HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2019.

**M**vuva zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa majili ya mazao na malisho. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuzitumia mvua hizi vizuri kwa shughuli za kilimo na mifugo. Vilevile wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki. Wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu

### HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2019

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kiasi katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la Ziwa Viktoria, Rufiji, Pangani na Wami/Ruvu. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz) (2) [agromet@meteo.go.tz](mailto:agromet@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)